# Maelezo ya mgonjwa wa VVU kwa watu wenye matibabu ya VVU iliyodhibitiwa vizuri

## Karatasi ya maelezo ya magonjwa ya kuambukiza

### Kwa nini umepewa maelezo haya?

Una ambukizo la VVU ambalo linatibiwa na madawa ya kupunguza makali ya virusi vya ukimwi na daktari wako amechunguza matibabu yako kuwa inadhibitiwa vizuri. Tiba ya VVU iliyodhibitiwa vizuri inamaanisha ya kwamba:

- Wingi wa virusi katika damu yako haitambuliki wakati wote.
- Wewe ni mwangalifu kuchukua dawa yako mara kwa mara na kama ilivyoagizwa.
- Wewe huhudhuria miada ya uchunguzi wa afya na matibabu, mara 2-4 kwa mwaka au kama ulivyoamuliwa na daktari wako.

### VVU ni nini?

VVU ni virusi vinavyoathiri mfumo wako wa kinga. Leo kuna dawa zinazopatikana ambazo, ikiwa zitatumiwa ipasavyo, zinaweza kupunguza wingi wa virusi katika mwili wako na kumwezesha mtu mwenye VVU kuishi maisha marefu na mazuri. Ikiwa una maambukizi ya VVU na matibabu iliyodhibitiwa vizuri hakuna hatari ya kuambukizana kwa njia ya kufanya ngono. Ambukizo la VVU halitibiwi kikamilifu na virusi hubakia katika mwili wako hata wakati matibabu yako inadhibitiwa vizuri.

### VVU huenezwaje?

Watu wengi ambao wana VVU wameambukizwa maambukizi kwa njia ya ngono isiyozuiliwa, kwa kawaida kupitia kufanya ngono ya uke au ya mkundu,lakini wakati mwingine kupitia ngono ya mdomo pia. Damu iliyo na VVU ni ya kuambukiza na VVU inaweza kupitishwa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine kupitia utiaji-damu mishipani, majeraha yanayosababishwa na sindano au kugawana sindano moja. Katika kisa cha matibabu ya VVU yenye kudhibitiwa vizuri, wingi wa virusi katika damu hupunguzwa kwa kadiri ambayo maambukizi haitokei kwa njia ya ngono. Linapokuja suala la maambukizi kwa njia ya damu (yaani kwa njia ya majeraha yanayosababishwa na sindano, kukatwa na kushiriki sindano moja), hatari ya ambukizo kutoka kwa mtu aliye na matibabu ya kudhibitiwa vizuri haijawahi pia kuchunguzwa na kwa hivyo uambukizi hauwezi kuondolewa kabisa. VVU inaweza kupitishwa kutoka kwa mama hadi mtoto wakati wa ujauzito, kujifungua na kunyonyesha. Ikiwa maambukizi ya mama aliye na VVU inajulikana basi hatari kwa mtoto inaweza kuondolewa kabisa kwa kutumia dawa na kujiepusha na unyonyeshaji.

**Wakati gani VVU haviambukizwi?**
VVU haiwezi kuambukizwa kwa kumkumbatia, kumbusu au kupapasa-papasa. Machozi, mkojo, kinyesi, matapiko na kamasi ambazo hazina damu hayawezi kueneza virusi. Damu inayogusana na ngozi ambayo ni thabiti na haijaharibiwa haina hatari ya maambukizi.

**Haki**
Kulingana na Sheria ya Kuambukiza Magonjwa nchini Sweden (Smittskyddslagen), kupima, kutembelea kliniki na matibabu ya VVU vyote ni bila malipo.
Pia una haki ya msaada wowote wa kisaikolojia wa kijamii ambao unaweza kuhitaji ili udhibiti ugonjwa wako. Daktari wako atakupa ushauri juu ya jinsi ya kuepuka kuwasababishia wengine kwa hatari ya maambukizi.

**Maisha ya kikazi**
Maambukizi ya VVU haiwezi kuweka vikwazo vyovyote kwenye masomo yako au maisha yako ya kikazi.

**Ujauzito na kunyonyesha**
Unaweza kupata msaada kwa ajili yako au mpenzi wako ili kupata mimba ya hatari ndogo za maambukizo kwa mtoto wako. Ili kulinda mtoto, wanawake wajawazito wanaoishi na VVU wanatakiwa kuwajulisha watoa huduma wao wa afya kuhusu maambukizi yao ya VVU katika hatua ya mapema ya ujauzito ili hatua za kuzuia ziweze kuchukuliwa. Wanawake wenye VVU wanashauriwa kutonyonyesha.

**Watoto wenye VVU**
Wazazi / walezi na watoto watapewa taarifa zinazofaa kulingana na umri juu ya maambukizi kwa ustadi na daktari wao. Watoto wenye VVU wana haki sawa ya kutunzwa na shule kama watoto wengine lakini wanaweza kuwa na mahitaji maalum ambayo yanapaswa kuzingatiwa. Daktari wako wa kukutibu au daktari wako wa magonjwa ya kuambukiza anaweza kutoa habari kwa shule ya chekechea ikiwa wazazi / walezi wametoa idhini yao kwa hili. Afya ya mwanafunzi inahitaji kujulishwa wakati mtoto anapoanza shule.

**Matumizi ya kondomu wakati wa kufanya ngono ya kike, ngono ya mkundu na ngono ya mdomo**
Kondomu hutoa ulinzi mzuri dhidi ya VVU na magonjwa mengine ya zinaa. Wakati tiba yako ya VVU inadhibitiwa vizuri, huwajibiki kutumia kondomu wakati unavyofanya ngono, lakini kufanya hata hivyo inapendekezwa kwa sababu inatoa ulinzi dhidi ya maambukizi mengine yanayoweza kuambukizwa.

**Damu lazima ionekane sikuzote kama yenye kuambukiza**

- Mtu yeyote ambaye anaweza kugusa damu yako (wakati anapotibu jeraha au sawa) lazima avae glavu.
- Ikiwa mtu amegusa damu yako (kwa mfano kupitia kidonda au kupitia jeraha linalosababishwa sindano au kukatwa), lazima umjulishe huyo mtu ya kuwa damu yako inaweza kusababisha hatari ya kuambukizwa VVU na kwamba anapaswa kuwasiliana na kliniki ya maambukizi / daktari wa kuitwa ili kufanyiwa tathmini.

**Kanuni za maadili ambazo unapaswa kufuata ili kuepuka kuambukiza wengine**
Kwa mujibu wa Sheria ya Kuambukiza Magonjwa, VVU hutambuliwa kama ugonjwa ambao unaleta hatari kwa umma. Kwa hivyo una wajibu kuzuia maambukizi kuenezwa kutoka kwako hadi kwa wengine. Ikiwa hatari ya kuambukizwa imetokea, lazima ujulishe huyo mtu mwingine kuhusu ugonjwa wako. Ifuatayo ni orodha ya sheria za mwenendo ambazo zinapaswa kufuatiliwa ili kuzuia maambukizi kulingana na maeneo yaliyozungumziwa katika sheria. Sheria nyingi zinatumika kwa kila mtu mwenye VVU ingawa baadhi zingine zinatumika katika hali maalum na zinaweza kubadilika kwa muda. Ni daktari wako ambaye anaamua ni sheria zipi zifuatazo zinatumika hasa kwako.

1. Huwezi kuchangia damu, viungo au tishu za kupachikwa mwilini.
2. Ikiwa unatumia sindano, bomba au vifaa vingine vya sindano kwa madhumuni ya matibabu, huwezi kuruhusu wengine kutumia vifaa hivyo.
3. Ikiwa unatumia sindano au bomba ya kuingiza madawa au vitu vinginevyo, huwezi kuruhusu wengine kutumia vifaa hivyo. Wala usitumie kikombe cha kuchanganya pamoja. Vifaa vyote vya sindano vinapaswa kuhifadhiwa na kutupwa kwa njia ambayo haina hatari ya kuambukizwa kwa wengine.
4. Unapotembelea mtoa huduma ya afya au daktari wa meno, lazima uwajulishe kwamba una maambukizi ya damu kabla ya hatua yoyote inayohusisha na hatari kubwa ya majeraha yanayosababishwa na sindano au kukatwa kabla kufanyika; k.m. hatua za upasuaji. Katika kisa cha uchunguzi rahisi wa kawaida katika huduma ya msingi na utaalamu wa meno, ikiwa ni pamoja na sampuli za damu na sindano, hautahitajika kutoa taarifa hii.
5. Usishiriki vifaa vya choo vinavyoweza kujereruhi kama vile nyembe
6. Lazima uhudhurie uchunguzi wa afya wowote ambao daktari wako anaona kuwa inafaa.

Ikiwa unadhani kuwa sheria yoyote ya maadili haya haitumiki kwako basi unaweza kuwasiliana na daktari wa magonjwa ya kuambukiza katika kata / eneo lako.